*Jarida La*

# MIFUGO NA UVUVI

*#mifugonauvuviniutajiri*

TOLEO NO; WMU 011| 2025 WWW.MIFUGOUVUVI.GO.TZ | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
MINISTRY OF LIVESTOCK AND FISHERIES

# Tanzania kutokomeza Kichaa cha Mbwa ifikapo 2030

*Yatajwa kuwa ya tatu mpango wa kudhibiti kichaa cha mbwa Afrika*





**UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025**
*Kura Yako Haki Yako, Jitokeze Kupiga Kura*

Septemba 2025

*Scan hapa Kusoma taarifa za Tovuti yetu*

@Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jarida la Mtandaoni

HALIUZWI

Toleo Na.011 | 2025

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi

# **Yaliyomo** Ndani **Jarida**


1 Bodi ya Uhariri............**Uk. 04**

2 Tanzania ya tatu Afrika mpango rasmi wa kudhibiti kichaa cha mbwa ............**Uk. 05 - 06**

3 Serikali, NMB kushirikiana kukuza sekta za mifugo na uvuvi.......**Uk 07**

4 Miradi kukamilishwa kwa wakati, kuleta tija kwa wananchi..... **Uk. 08-09.**

5 Kongamano la kwanza la Nguruwe Afrika lafanyika Tanzania ........... **Uk. 09**

6 Mifugo na Uvuvi yahitimisha SHIMIWI 2025 kwa kishindo........... **Uk. 09**

7 Matukio katika picha maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Kitaifa 2025 mkoani Manyara... **UK. 10**

8 Tanzania yafungua milango ya uwekezaji sekta za mifugo na uvuvi kimataifa ........... **Uk. 11**

9 Serikali yalifungua Ziwa Ikimba kwa mafanikio....... **Uk. 12**

10 Serikali yamkabidhi mkandarasi mradi wa Bil. 1.3 Pangani ......... **Uk. 13**

11 Serikali imelenga kuiinua sekta ya maziwa nchini - Dkt. Mhede.......... **Uk. 14**

12 Zao la mwani kuingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani ....**Uk. 15**

13 Serikali, Heifer International kuongeza wigo programu ya BBT ........**Uk. 15**

14 UNDP, Wizara ya Mifugo na Uvuvi zapandikiza vifaranga elfu 10 vya samaki Ziwa Victoria ........**Uk. 16**

15 TSAP ni kielelezo cha maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi - Bi. Meena ........**Uk. 17**

16 Tanzania yazindua rasmi mradi wa STOSAR II ........**Uk. 18 - 19.**

17 Ujumbe wa Tanzania washiriki Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika nchini Senegal .......**Uk. 19**

18 Tanzania yaikaribisha Oman kuwekeza kwenye sekta za mifugo na uvuvi .......**Uk.20**

19 Matukio mbalimbali katika picha........... **Uk. 21 - 22**
















# Bodi ya Wahariri:

## Mwenyekiti
**Mbaraka Kambona**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

## Mhariri
**Edward Kondela -** Afisa Habari Mwandamizi

## Msanifu
**Hamisi Hussein** - Afisa Habari

## Wajumbe
**Elibariki Mafole -** Afisa Habari Mwandamizi
**Omary Mtamike -** Afisa Habari Mwandamizi
**Stanlay Bryaton -** Afisa Habari
**Chiku Makwai-** Afisa Habari
**Martha Mbena** - Afisa Habari



# TANZANIA YA TATU AFRIKA MPANGO RASMI WA KUDHIBITI KICHAA CHA MBWA

## Mbwa 3,653 Paka 212 wakipewa chanjo ya kichaa cha Mbwa wilayani Kiteto.

**Na Chiku Makwai**

Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa afya ya wanyama imeandaa mpango rasmi wa kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa ikiwa ni moja ya mkakati wa kufikia azma ya Dunia ya kuondokana kabisa na ugonjwa huo ifikapo Mwaka 2030.

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi Agnes Meena katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Kitaifa yaliyofanyika Septemba 29, 2025 Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara.

Bi. Meena amesema mpango huo ambao umeshapitiwa na kuridhiwa na Shirika la Afya ya Wanyama duniani (WOAH) utaratibu uchanjaji wa mbwa na paka wote nchini kwa muda wa miaka mitano.

"Kupitia mpango huo, ni imani yetu kwamba hadi kufikia Mwaka 2030 Tanzania itakua ni miongoni mwa nchi zitakazokuwa zimeutokomeza ugonjwa huu wa Kichaa cha Mbwa",amesema Bi Meena.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi kutoa taarifa kwa wataalam wa mifugo walio karibu yao au serikali ya mtaa ya eneo husika endapo watakutana na mnyama au mfugo wenye dalili zisizo za kawaida.

"Kwa hiyo lengo la maadhimisho haya ambayo yamesababisha tukusanyike hapa leo ni kukumbushana na kuelimishana zaidi jinsi ya kukabiliana na janga hili la ugonjwa wa kichaa cha mbwa", amesema Bi. Meena.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Benezeth Lutege amebainisha kuwa takwimu zinaonesha mpaka kufikia Septemba 29, 2025 wilayani humo wametoa chanjo kwa mbwa 3653, paka 212, kuhasi mbwa 96, paka 5 na kufunga vizazi vya mbwa 52 na paka 26.

Akisoma taarifa kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Katibu Tawala wa wilaya hiyo Bi. Mufandii Msaghaa amesema serikali imekuwa ikitekeleza utoaji wa chanjo kwa mifugo na wanyama kwa lengo la kuikinga dhidi ya magonjwa na kwamba mchakato huo ni sehemu ya utekelezaji wa sera za mifugo hapa nchini.

Endelea Ukurasa. 06 >>>

>>> Kutoka UK. 05

# Tanzania ya tatu Afrika mpango rasmi wa kudhibi kichaa cha mbwa

Nao baadhi ya wananchi ambao ni wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto wameishukuru serikali kwa kuja na mpango mkakati wa kudhibiti kichaa cha mbwa kupitia chanjo zinazotolewa na kutoa ombi la kuwafikia wananchi waliokando ya mji hasa maeneo ya vijijini ili kuwakinga dhidi ya ugonjwa huo.

Maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Kitaifa kwa Mwaka 2025 yameenda sambamba na kauli mbiu isemayo Kichaa cha Mbwa; "Chukua Hatua Sasa, Mimi, Wewe na Jamii."






Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Dk. Benezeth Lutege (watatu, kulia) akimwelezea Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena (Wapili Kulia) jinsi chanjo ya kichaa cha mbwa inavyotolewa ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Kitaifa iliyofanyika Kiteto Manyara Septemba 29, 2025.



# SERIKALI, NMB KUSHIRIKIANA KUKUZA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

**Na, Martha Mbena**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema itaendeleza ushirikiano na benki ya NMB kutekeleza vipaumbele vya sekta ya mifugo na uvuvi vya mwaka 2025/2026 ili kufanya mageuzi ya kiuchumi nchini.

Hayo yamebainishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena Septemba 26.2025 mara baada ya kukutana ofisini kwake Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma, na kufanya mazungumzo yenye lengo la kuutambulisha uongozi wa benki hiyo mkoa wa Dodoma na kuwasilisha mikakati iliyowekwa na NMB kwa ajili ya kuchangia ukuaji wa sekta ya mifugo na uvuvi.

> *"Niwahakikishieni ushirikiano mkubwa benki ya NMB kwa kuendelea kufanya kazi katika shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi."*
>
> Bi, Agnes Meena - Katibu Mkuu

"Niwahakikishieni ushirikiano mkubwa benki ya NMB kwa kuendelea kufanya kazi katika shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi." Amesema Bi. Meena

Katika mazungumzo hayo, Bi. Meena amejadiliana maeneo ya kushirikiana kati ya benki hiyo na wizara na kutaja vipaumbele vinne vya wizara kuwa ni kukuza uzalishaji, uuzaji na uongezaji wa mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo na uvuvi, kuimarisha ulinzi na usimamizi endelevu wa rasilimali za sekta ya mifugo na uvuvi, kukuza uwekezaji katika sekta ya mifugo na uvuvi na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Huduma za Serikali kutoka benki ya NMB, Bi. Vicky Bishubo amempongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuteuliwa na kufanya kazi kwa bidii katika sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Bi. Bishubo ametaja na kuainisha mafanikio na shughuli zinazofanywa na benki hiyo kwenye maeneo mbalimbali kama minada ya mifugo, vikundi vya ushirika vya wafugaji ambapo kupitia shughuli hizo za benki wafugaji wamekuwa wakiitumia kutekeleza shughuli za kisekta kwa manufaa ya nchi.

# MIRADI KUKAMILISHWA KWA WAKATI, KULETA TIJA KWA WANANCHI



**Na, Edward Kondela**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeombwa kuendelea kusimamia vyema miradi inayotekelezwa nchini kwa kuhakikisha inakamilika kwa wakati na inakuwa na tija kwa wananchi.

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Dkt. Mussa Ali Mussa amebainisha hayo Septemba 8, 2025 ofisini kwake, wakati akipatiwa taarifa juu ya maboresho na ujenzi wa baadhi ya miundombinu katika kituo kikubwa cha kuendeleza ukuzaji viumbe maji cha Kingolwira pamoja na kituo kidogo cha Boma Road.

Dkt. Mussa amesema miradi inayoibuliwa katika Mkoa wa Morogoro ni vyema iwe inakamilika kwa wakati na endapo kama kuna changamoto zozote katika utekelezaji wake, wizara isisite kuwasiliana na ofisi yake ili kuhakikisha zinatatuliwa.

Akizungumza mara baada ya kumkabibidhi makandarasi maeneo ya utekelezaji wa miradi mitatu, katika kituo kikubwa cha kuendeleza ukuzaji viumbe maji cha Kingolwira na kituo kidogo cha Boma Road, Mkurugenzi wa Kuendeleza Miundombinu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mhandisi George Kwandu, amesema miradi hiyo inagharamu shilingi milioni 368.1.

Miradi inajumuisha uchimbaji wa visima viwili vya maji pamoja na kufunga pampu katika vituo hivyo; ukarabati wa jengo la kitotoleshi la vifaranga vya samaki na ujenzi wa mfumo wa kurejeleza maji kwenye kitotoleshi katika kituo kikubwa cha Kingolwira.

Aidha, ameongeza kuwa katika kituo kidogo cha Boma Road, unatekelezwa mradi wa ujenzi wa jengo la nishati ya umeme na kwamba miradi yote itatekelezwa katika kipindi cha miezi mitatu hadi kukamilika.

Amefafanua kuwa kukamilika kwa miradi hiyo, vituo hivyo vitaongeza uzalishaji na kufikia vifaranga milioni moja kwa mwezi hivyo kutaka makandarasi kuhakikisha wanazingatia mikataba na kukamilisha kazi kwa wakati.

Kwa upande wake Afisa Uvuvi Mkoa wa Morogoro, Bi. Scontina Mgina amesema maboresho yanayofanyika yatasaidia mkoa huo na mikoa ya jirani katika upatikanaji wa vifaranga vya samaki vya kutosha kwa kuwa watu wengi wamehamasika katika ufugaji wa samaki.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya EF IMER Construction Ltd, Bw. Emmanuel Pallangyo akiwa ni mmoja wa makandarasi watatu waliokabidhiwa maeneo ya ujenzi na ukarabati katika kituo kikubwa cha kuendeleza ukuzaji viumbe maji cha Kingolwira na kituo kidogo cha Boma Road, ameishukuru Serikali kwa kuwapatia wazawa kutekeleza miradi hiyo na

kwamba wataikamilisha kwa wakati.

Miradi ya maboresho na ujenzi wa baadhi ya miundombinu katika kituo kikubwa cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira pamoja na kituo kidogo cha Boma Road, inatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) chini ya uratibu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

## Kongamano la kwanza la Nguruwe Afrika lafanyika Tanzania

**Na, Martha Mbena**

Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mizengo Pinda amesema Kongamano la Nguruwe Afrika limelenga kuonesha fursa mbalimbali zilizopo katika mnyororo wa thamani wa nguruwe, kukutanisha wadau na kubadilishana uzoefu.

Akifungua Kongamano hilo lililofanyika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania katika Jiji la Dar es Salaam Septemba 11, 2025, Mhe. Pinda alisema Tanzania imepata fursa ya kipekee ya kuwa mwenyeji wa kongamano hilo la kimataifa ambalo litatumika kuonyesha fursa za uwekezaji zilizopo katika tasnia ya nguruwe, kuongeza wigo wa masoko ya nguruwe na bidhaa zake katika nchi za Afrika.

“Tukio hili sio tu mkusanyiko wa wataalam, wakulima, wawekezaji na watunga sera bali ni sherehe ya sekta ambayo inabadilisha maisha ya wananchi katika taifa letu, kwa hiyo Tanzania imepata fursa ya kipekee ya kuongeza fursa ya mnyororo wa thamani wa nguruwe.” amesema Mhe. Pinda.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena amesema Serikali ya Tanzania imejipanga kuimarisha huduma za mifugo, utafiti na ushirikiano na sekta binafsi ili kuinua uzalishaji wa nguruwe nchini.

“Kongamano hili linawaleta wadau mbalimbali kwa lengo la kukutana na kujadiliana kuhusiana na changamoto zilizopo kwenye ufugaji wa nguruwe kwa ajili ya kuzitafutia majibu kwa pamoja” alisema Bi. Meena.

Pia, amesema serikali itaendelea kutoa tiba kwa kwa nguruwe na kufanya tafiti mbalimbali zitakazosaidia kuboresha ufugaji na kuwezesha kuwaunganisha wafugaji wa ndani na nje ya nchi ili kuweza kupata masoko.

## Mifugo na uvuvi yahitimisha SHIMIWI 2025 kwa kishindo!

**Na, Omary Mtamike**

Timu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imehitimisha michuano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali nchini (SHIMIWI) iliyokuwa ikifanyika kwenye viwanja mbalimbali jijini Mwanza kwa kishindo baada ya kufanikiwa kunyakua kombe na medali mbili kwenye michezo iliyocheza wakati wote wa michuano hiyo.

Timu hiyo imefanikiwa kubeba kombe la mchezo wa bao upande wa wanawake ambapo mchezaji Jamila Kalambo alinyakua ubingwa wa mchezo huo baada ya kumshinda Laina Abbas kutoka Wizara ya Maji.

Aidha, timu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliibuka mshindi wa pili na tatu upande wa mchezo wa kurusha tufe kwa wanawake na wanaume na kufanikiwa kubeba medali mbili katika mchezo huo.

Katika hatua nyingine wizara hiyo imefanikiwa kushika nafasi ya nne kwenye mchezo wa kuvuta kamba (wanaume) huku timu hiyo ikitajwa kama timu yenye ushindani wakati wote wa michuano hiyo baada ya kufanya hivyo pia katika misimu miwili iliyopita.

Michuano hiyo ambayo hufanyika kila mwaka imehitimishwa rasmi Septemba 16, 2025 ambapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeahidi kurejea imara zaidi kwenye michuano ijayo.



# MATUKIO KATIKA PICHA

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Kitaifa iliyofanyika Kiteto - Manyara ambapo Katibu Mkuu Bi. Agnes Meena alikuwa Mgeni Rasmi Tarehe 29 Septemba, 2025














## TANZANIA YAFUNGUA MILANGO YA UWEKEZAJI SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI KIMATAIFA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena amenadi fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta za mifugo na uvuvi nchini Tanzania.

Tukio hilo limefanyika wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika katika chumba maalum cha kunadi fursa kijulikanacho kama Deal Room Septemba 4, 2025 katika jiji la Dakar nchini Senegal.

Bi. Meena ameelezea kuwa Tanzania ina fursa adhimu zinazochochea uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi zikiwemo utajiri wa rasilimali zinazochangia uhakika wa malighafi viwandani, uwepo wa maji ya asili ya kutosha kama vile bahari, mito na maziwa ambayo yanawezesha shughuli za uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji na uwepo wa maeneo kwa ajili ya ufugaji na uzalishaji wa malisho kibiashara.

Vilevile, Bi. Meena alieleza kuwa Tanzania ina soko lililo tayari kwa bidhaa zitakazozalishwa kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya watu pamoja nafasi ya kijiografia ya nchi inayowezesha kuyafikia kirahisi masoko ya kikanda na kimataifa

Akielezea fursa zilizopo Bi. Agnes Meena amebainisha maeneo ya kimkakati ya uwekezaji ambayo ni eneo la nyama, maziwa, kuku, vyakula vya mifugo na samaki, ukuzaji wa viumbe maji na uongezaji wa thamani kwa mazao ya mifugo na uvuvi.






## Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendeleza ushirikiano na ILRI miradi ya kimkakati

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena amekutana na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Dkt. Siboniso Moyo Septemba 5, 2025, mara baada ya kumalizika kwa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika uliofanyika jijini Dakar nchini Senegal.

Katika kikao hicho, viongozi hao wamekubaliana kushirikiana katika kuimarisha ushiriki wa vijana kwenye miradi ya kuku, ufugaji wa samaki, uzalishaji wa chakula cha mifugo na samaki, pamoja na kushirikiana na sekta binafsi katika uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho.

ILRI pia imeahidi kuiunganisha wizara na wadau wa wengine wa maendeleo ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa kampeni ya chanjo.

Vilevile, taasisi hiyo imekubali ombi la Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi la kuongeza ajenda ya uvuvi katika kikao cha Mawaziri wa Mifugo kinachojulikana kama Livestock Ministerial Deep Dive" ambacho hufanyika ndani ya Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika.



# Serikali yafungua Ziwa Ikimba kwa mafanikio

## Uzalishaji wa samaki waongezeka kutoka tani 1.5 kwa mwaka hadi tani 15





**Na, Omary Mtamike**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imelifungua Ziwa Ikimba lililopo mkoani Kagera ikiwa ni miezi 6 tangu ilipolifunga kwa lengo la kuongeza kiwango cha samaki kwenye ziwa hilo.

Akizungumza wakati wa hafla ya kufungua ziwa hilo Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Mhe. Erasto Sima ambaye alimwakilisha mkuu wa mkoa wa Kagera Mhe. Fatma Mwasa amewataka wananchi wanaonufaika na uvuvi wa ziwa hilo kutoacha shughuli walizokuwa wakizifanya wakati wote wa ufungaji wa ziwa ili kuwa na uchumi jumuishi kwenye eneo hilo.

"Niwapongeze sana kwa kutii makubaliano ya kutofanya shughuli za uvuvi katika kipindi chote cha ufungaji wa ziwa na leo sote tumeshuhudia matunda ya uvumilivu wenu." Amesema Mhe. Sima.

Aidha, Mhe. Sima amesema kuwa ufunguzi wa ziwa hilo utaongeza mapato ya halmashauri ambapo mpaka sasa takriban shilingi milioni 8 zimeshapatikana kupitia usajili wa mitumbwi ya kuvulia samaki pekee.

"Lakini pia ni muhimu tujiwekee mazoea ya kufunga ziwa angalau kwa miezi 6 ili kuendelea kunufaika na rasilimali za uvuvi zinazotokana na ziwa letu na kuendelea kukuza uchumi wetu." Ameongeza Mhe. Sima.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede amesema kuwa wizara itaendelea kuchagiza shughuli za uvuvi kwenye ziwa hilo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wavuvi ili kufanya uvuvi unaokubalika kisheria na kuongeza takriban vifaranga Mil.1 vya samaki kabla ya mwisho wa Mwezi Oktoba mwaka huu.

"Wataalam wetu wa wizara wataweka kambi hapa kwa ajili ya kutoa elimu hiyo kwa kukaa na nyie darasani ili kuwaelimishana kuhusu uvuvi unaofaa." Amesema Dkt. Mhede.

Akielezea hali ya upatikanaji wa samaki ilivyo hivi sasa kwenye ziwa hilo, Mkurugenzi wa Uvuvi nchini, Prof. Mohammed Sheikh amesema kuwa kwa mujibu wa utafiti wa kitaalam uliofanyika leo ziwani hapo, kiwango cha mavuno ya samaki kwa mwaka kinatarajia kupanda kutoka tani 1.5 hadi kufikia tani 15 huku kiwango hicho kikitarajiwa kuongezeka zaidi endapo rasilimali za uvuvi zilizowekwa ziwani humo zitalindwa kikamilifu.

"Huu ni mkakati wa serikali wa kuhakikisha kwamba uzalishaji unaongezeka, wananchi wanapata tija na mchango wa sekta ya uvuvi kwenye pato la Taifa unaongezeka." Amesema Prof. Sheikh.

Kwa upande wao wavuvi wanaonufaika na Ziwa hilo, Bw. Benickson Charles na Bi. Rehema Hamza wamesema kuwa kufunguliwa kwa ziwa hilo na kuongezeka kwa kiwango cha samaki wanaopatikana ni fursa ya wao kukuza uchumi wao.

Ziwa Ikimba lilifungwa Machi 12, 2025 kwa makubaliano ya hiyari baina ya Serikali, wavuvi na wananchi wanaonufaika, kwa lengo la kuongeza kiwango cha uzalishaji wa samaki ili kukuza uchumi kwa wakazi wa eneo hilo, mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla.

> *"Ni muhimu tujiwekee mazoea ya kufunga ziwa angalau kwa miezi 6 ili kuendelea kunufaika na rasilimali za uvuvi zinazotokana na ziwa letu na kuendelea kukuza uchumi wetu."*
>
> Dkt. Edwin Mhede
> Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi



# Serikali yamkabidhi mkandarasi mradi wa bil. 1.3 Pangani

**Ni kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi, Halmashauri ya Pangani kuinua uchumi wa wavuvi**

**Na, Martha Mbena**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) inayofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) imekabidhi ujenzi wa soko la samaki katika Kata ya Kipumbwi, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani mkoani Tanga wenye thamani ya shilingi bililioni 1.3 kwa mkandarasi.

Akiongea wakati wa kukabidhi mradi huo Septemba 17, 2025, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena amesema soko hilo ni matokeo ya dhamira ya serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha sekta ya uvuvi inakua kwa tija, inachangia pato la taifa na pia inaboresha maisha ya wananchi.



Bi. Meena amesema kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inalenga kuwapatia wavuvi miundombinu ya kisasa ya kupokea, kuhifadhi na kuchakata samaki kwa kuzingatia ubora na usalama wa mazao ya uvuvi, lengo ikiwa ni kupunguza upotevu, kuongeza thamani, kukuza biashara na kuimarisha mapato ya wananchi na serikali kwa ujumla.

"Mradi huu ni kielelezo cha dhamira ya serikali ya kuboresha sekta ya uvuvi ikiwa ni pamoja na kuboresha maisha ya wananchi na kuongeza mchango kwenye pato la taifa." Amesema Bi. Meena.

Pia, Bi. Meena amesema wizara kwa kushirikiana na viongozi wa Mkoa wa Tanga itasimamia mradi huo kikamilifu ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na kwa viwango ambavyo vimekusudiwa.

Aidha, wizara itaendelea kuwekeza katika miradi mingine ya uvuvi Wilaya ya Pangani na katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Batilda Burian amesema mradi wa ujenzi wa soko la samaki Kipumbwi ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chaa cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025 ambayo inaelekeza serikali kuboresha na kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya uvuvi ili kuongeza tija na kipato cha wananchi.

"Sote tunafahamu kuwa idadi ya watu wanaojipatia kipato kupitia shughuli za uvuvi nchini imeendelea kuongezeka kutoka watu milioni 4.5 Mwaka 2020 hadi zaidi ya milioni 6 Mwaka 2025, hivyo mkandarasi ufanye kazi kwa kuzungatia ubora na muda uliopangwa." Amesema Mhe. Burian

Naye, Mwenyekiti wa chama cha ushirika cha wavuvi na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi wa Kata ya Kipumbwi, Bw. Said Issa ameishukuru serikali kwa kuwaletea soko la dagaa la kimataifa kwa kuwa soko hilo litakuwa mkombozi kwao kwa kuwasaidia kupata bei nzuri.

> “Mradi huu ni kielelezo cha dhamira ya serikali ya kuboresha sekta ya uvuvi ikiwa ni pamoja na kuboresha maisha ya wananchi na kuongeza mchango kwenye pato la taifa.
>
> **Bi. Agnes Meena**
> **Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

# SERIKALI IMELENGA KUIINUA SEKTA YA MAZIWA NCHINI - DKT. MHEDE

**Na, Hamisi Hussein**



Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imelenga kuiinua sekta ya maziwa nchini kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo mafunzo ya uongezaji thamani yanayotolewa kwa wafugaji nchini ili sekta hiyo ya maziwa iweze kuongeza mchango katika pato la taifa na kuinua uchumi wa wafugaji.

Akizungumza Septemba 9, 2025 wakati akifunga mafunzo ya mradi wa Maziwa Faida kwa wafugaji wa Halmashauri ya wilaya ya Muheza mkoani Tanga unaolenga ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede amewataka watekelezaji wa mradi huo ikiwemo Wakala ya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA) na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kwa kushirikiana na wadau kuhakikisha unawafikia wanufaika wote wa mradi huo kwa kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali yakuongeza thamani ya sekta ya mifugo.

"Maelekezo ya serikali hata dhamira zetu, asikosekane hata mfugaji mmoja kuifikia idadi ya wafugaji 3,000 ili kuhakikisha malengo ya mradi wetu yanafikiwa kama ilivyokusudiwa, kwahiyo mafunzo haya yawe endelevu." Alisema Dkt. Mhede



Pamoja na maelekezo hayo Dkt. Mhede amewahimiza wafugaji na wananchi kwa ujumla kunywa maziwa angalau nusu lita kwa siku kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula na kuwaagiza watekelezaji wa mradi wa Maziwa Faida kuzishirikisha taasisi za fedha na bima ili zitoe elimu ya kuongeza thamani ya mifugo na mazao yake kwa kufanya ufugaji endelevu wenye tija.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa LITA, Dkt. Pius Mwambene amesema ni wakati sasa wafugaji kuwa tayari kubadilisha mifumo ya ufugaji ili kuendana na ufugaji utakaongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo ili kuvihudumia viwanda hapa nchini na kuzalisha ajira kwa wananchi.

Naye Mratibu Mkuu wa mradi wa Maziwa Faida, Dkt. Zabron Nziku amesema mradi huo umefadhiliwa na serikali ya Ireland na unatekelezwa na Mamlaka ya Utafiti Ireland (TEAGASC), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) na Wakala ya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA).

Mradi huu unagharimu Shilingi Bilioni 7 na utatekelzwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/2022 hadi 2025/2026 na hadi kufikia Mwezi Juni mwaka huu jumla ya wafugaji 2,239 wamefikiwa na mradi huku lengo ni kuwafikia wafugaji 3,000.

Hata hivyo Wizara imeendelea kuimarisha biashara ya maziwa ambapo mwaka 2024/2025 jumla ya lita za maziwa 90,416,788.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 226 zilisindikwa na kuuzwa katika masoko ya ndani ya nchi.



# SERIKALI, HEIFER INTERNATIONAL KUONGEZA WIGO PROGRAMU YA BBT

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena, amekutana na Bi. Adesudwa Ifedi, Makamu wa Rais wa Shirika la Heifer International anayesimamia Programu za Afrika, tarehe 5 Septemba 2025 jijini Dakar, Senegal, kando ya Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika.



Katika mazungumzo hayo, viongozi hao wamejadili kuhusu kupanua wigo wa Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) ili kuwafikia vijana wengi zaidi nchini, pamoja na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa programu hiyo, kwa lengo la kuongeza ufanisi na uendelevu wake.

Kwa upande wake, Bi. Ifedi ameipongeza wizara kwa ushirikiano mzuri, na amemuelekeza Mkurugenzi wa Heifer International Tanzania, Bw. Mark Txoso, kuendelea kushirikiana na wizara katika kubainisha vipaumbele vilivyojadiliwa ili viweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu za shirika hilo.

Vilevile, ameishukuru serikali kwa kuitambua Heifer kama mmoja wa wadau muhimu wa maendeleo nchini.



## Zao la mwani kuingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia idara ya ukuzaji viumbe maji kwa kushirikiana na bodi ya usimamizi wa stakabadhi za ghala imeanza mazungumzo ya kuja na mfumo wa stakabadhi ghalani kwa zao la mwani ili kuimarisha bei ya zao hilo.

Mazungumzo hayo yalifanyika Septemba 17, 2025 baada ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian kukutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Bw. Bangu Asangye na Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt Nazael Madalla.

Mfumo huo umelenga kufanya kazi katika Wilaya za Pangani, Mkinga na Tanga ambayo ni maeneo muhimu katika uzalishaji wa mwani.

Mfumo wa stakabadhi ghalani unatarajiwa kuimarisha bei ya mwani, uhakika wa soko na kuondoa unyonyaji kutoka kwa madalali.

Mbali na mazungumzo hayo pia, Dkt. Burian ametoa wito kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuendelea kuwajengea uwezo wavuvi wa Mkoa wa Tanga kupitia miradi ya kiuchumi kama ufugaji wa samaki kwenye vizimba ili kuongeza kipato na kuboresha maisha yao.





# UNDP, Wizara ya Mifugo na Uvuvi zapandikiza vifaranga elfu 10 Ziwa Victoria

**Na, Edward Kondela**

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi limepandikiza vifaranga vya samaki 10,000 aina ya sato ndani ya Ziwa Victoria ikiwa ni mkakati wa kukuza Uchumi wa Buluu nchini kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2020-2050.

Akizungumza (18.09.2025) wakati wa ziara ya kikazi mkoani Mwanza, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede amesema UNDP imeonesha utayari wa kuungana na serikali katika mpango mkubwa wa kuendeleza Uchumi wa Buluu.

Dkt. Mhede ameongeza kuwa, kupandikizwa kwa vifaranga hivyo kwenye Ziwa Victoria, katika Mwalo wa Shadi, Kata ya Luchelele jijini Mwanza ni moja ya mikakati ya serikali kuhakikisha uwepo wa samaki ndani ya ziwa hilo.

"Tulianza kampeni ya kupandikiza vifaranga vya samaki aina ya sato, jambo lililomvutia Mkurugenzi Mkazi wa UNDP Tanzania, kufika eneo hili kupanda na sisi, zoezi hili ni endelevu." amesema Dkt. Mhede

Aidha, Dkt. Mhede ameishukuru Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kwa kutoa vifaranga hivyo, huku akifafanua kuwa miradi yote haiwezi kufanywa na serikali pekee bali inahitaji usaidizi wa aina nyingi ikiwemo mifumo ya maabara, mifumo ya kuzalisha vifaranga pamoja na kufikia hitaji kubwa kwenye kufuga samaki kwa njia ya vizimba na kulilisha Ziwa Victoria lenyewe.

Pia, amesema kunahitajika uwepo wa vifaranga vingi vya samaki pamoja na ubunifu kwa watendaji na watumishi wengine kuwa na rasilimali za pamoja za kuendeleza maeneo ya kando mwa Ziwa Victoria.

Halikadhalika, Dkt. Mhede ametoa wito kwa wananchi wote pamoja na wavuvi kutoingilia maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kuzalishia na kukuzia samaki kwa sababu ni kinyume kisheria na kuwataka wananchi wanaoishi maeneo hayo, kutoa taarifa panapotokea hali kama hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkazi wa UNDP Tanzania, Bw. Shigeki Komatsubara amewaasa wananchi kutumia vyema mazingira ya Ziwa Victoria kwa kuvua samaki kwa kufuata utaratibu uliowekwa na kwamba watakuwa mfano mzuri kwa nchi na wao wenyewe kujipatia faida.

Bw. Komatsubara amefafanua kuwa, katika ziara hiyo imempa changamoto ya kuanza kutafakari namna UNDP inapoweza kuchangia katika maeneo ambayo serikali kwa kushirikiana na wananchi tayari wameanza kuyasimamia katika Sekta ya Uvuvi.

Amesema UNDP itaendelea kufanya mazungumzo na serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kuhakikisha maeneo yatakayochochea ukuaji wa Uchumi wa Buluu yanaboreshwa zaidi.

Naye Katibu Mkuu wa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) Mwalo wa Shadi, Bw. Laurent Rusato akisoma risala ya kikundi hicho amesema wamepata mafanikio katika kudhibiti uvuvi haramu kwenye mwalo huo.

Aidha, ameiomba UNDP na serikali kuwaongezea nguvu ya kupata vifaa vya kisasa zaidi ili kuendelea kulinda rasilimali za uvuvi na kufanyika kwa uvuvi wenye tija na endelevu.

Katika ziara ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede na Mkurugenzi Mkazi wa UNDP Tanzania, Bw. Shigeki Komatsubara, wamefika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na kukutana na Katibu Tawala wa mkoa huo, Bw. Balandya Elikana pamoja na kutembelea Mwalo wa Igombe (Kayenze ndogo) uliopo wilayani Ilemela ili kujionea chanja za kukaushia dagaa, kutembelea mtambo wa kukaushia dagaa kwa njia ya jua wa Kampuni ya Millenium Engineers pamoja na eneo la mazalia ya samaki kwenye Ziwa Victoria katika Wilaya ya Nyamagana.

Pia, wametembelea Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) na Maabara ya Taifa ya Uvuvi (NQFL) ili kujionea baadhi ya shughuli wanazofanya katika kukuza Sekta ya Uvuvi kwa kuzingatia viwango vya ubora.



# TSAP ni kielelezo cha maendeleo ya mifugo na uvuvi - Bi. Meena

**Na, Omary Mtamike**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bi. Agnes Meena amesema kuwa Kongamano la Kisayansi la Chama cha Wataalam wa Sekta za Mifugo na Uvuvi (TSAP) ni kielelezo cha maendeleo ya sekta hizo.

Bi. Meena amebainisha hayo Septemba 24,2025 jijini Arusha alipokuwa akifungua kongamano la 48 la kisayansi la wataalam hao ambalo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kujadili taarifa za kitafiti zilizofanywa na wataalam hao kwa mwaka mzima na kupata ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hizo.

"Sekta hizi mbili ndo nguzo kuu za uchumi na lishe nchini kwani zina nafasi kubwa katika kuongeza pato la Taifa, ajira na usalama wa nchi" Amesema Bi. Meena.

Aidha Bi. Meena ameongeza kuwa kutokana na muktadha huo kongamano hilo limekuwa jukwaa la kimataifa la kubadilishana maarifa, uzoefu na mbinu bunifu za kuhakikisha kunakuwepo na uzalishaji wa tija na mwendelezo wa rasilimali za mifugo na uvuvi.

"Hivyo wafugaji na wazalishaji wanahimizwa kuwekeza katika teknolojia za kisasa na vitendea kazi sahihi vitakavyoongeza uzalishaji wenye tija katika sekta za mifugo na uvuvi" Amesisitiza Bi. Meena.

Awali akizungumza kwenye kongamano hilo Mwenyekiti wa TSAP, Dkt. Jonas Kizima amesema kuwa mkutano huo huambatana na malengo makuu manne ambayo ni kuhimiza maendeleo katika sayansi ya uzalishaji kwenye sekta za Mifugo na Uvuvi, kutoa fursa kwa wadau wa sekta hizo kukutana kila mwaka na kubadilishana mawazo, kuboresha ushirikiano wa watalaam wa ndani na nje ya nchi na kushirikiana na vyama vya wataalam wa sekta hizo ndani na nje ya nchi jambo ambalo huibua miradi mbalimbali ya kimataifa inayohusu sekta za Mifugo na Uvuvi.

Naye Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo kutoka Zanzibar, Dkt. Talib Suleiman amesema takriban asilimia 80 ya mifugo inayosindikwa visiwani humo inatoka Tanzania bara,Hivyo amewataka wafugaji na wataalam wa malisho nchini kutumia fursa ya soko kubwa la mazao hayo lililopo visiwani humo.

Chama cha Wataalam wa Sekta za Mifugo na Uvuvi (TSAP) kilianzishwa mwaka 1973 ambapo wataalam hao hukutana kila mwaka na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya sekta hizo.



> *Wafugaji na wazalishaji wanahimizwa kuwekeza katika teknolojia za kisasa na vitendea kazi sahihi vitakavyoongeza uzalishaji wenye tija katika sekta za mifugo na uvuvi*
>
> Bi. Agnes Meena
> Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi




# TANZANIA YAZINDUA RASMI MRADI WA STOSAR II

## Lengo ni kuboresha usalama na ubora wa chakula

**Na, Daudi Nyingo**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), imezindua rasmi Mradi wa STOSAR II unaolenga kuimarisha mifumo ya Sanitary and Phytosanitary (SPS) katika ukanda wa SADC ili kuwezesha biashara salama, ushindani na uendelevu wa mazao ya kilimo na vyakula.

Akizindua mradi huo Septemba 1, 2025 katika Hoteli ya Four Points by Sheraton jijini Dar es Salaam Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede alisema mradi huo utashughulikia maeneo muhimu yakiwemo afya ya wanyama, afya ya mimea, lishe na maendeleo ya minyororo ya thamani, hususan katika nyanja za uchunguzi na ufuatiliaji wa magonjwa, udhibiti wa ubora na upatikanaji wa masoko ya kikanda na kimataifa.

"Mkutano huu ni tukio mahususi la kuzindua mradi wa kikanda ambao Tanzania ni miongoni mwa wanufaika, mradi huu unalenga kuimarisha mifumo ya usafi na usalama wa chakula, simaanishi tu vyakula vya kawaida, bali pia mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia afya na usalama wa walaji, kwa lugha ya kitaalamu tunasema Sanitary and Phytosanitary Measures (SPS)" alisema Dkt. Mhede.

Alisema utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo uliyoanza Mwaka 2018 ambapo zaidi ya wataalamu 150 wa Tanzania tayari wamenufaika kwa kupata mafunzo, ingawa utekelezaji ulikumbwa na changamoto kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 (COVID-19).

Kwa upande wake, Mkuu wa Rasilimali Asilia katika Ujumbe wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania (EU), Bw. Lamine Diallo alisema Umoja wa Ulaya umekuwa mshirika wa kudumu katika kilimo cha ukanda huu ikiwemo Tanzania kupitia programu mbalimbali za kuongeza uzalishaji, kukuza mbinu za kilimo zinazoangalia mabadiliko ya tabianchi, kuboresha afya ya mimea, na kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha na masoko ya kikanda na kimataifa.

"Awamu hii mpya inajengwa juu ya mafanikio makubwa ya STOSAR I ambayo ilikamilika 2024 na kupitia STOSAR II maono yetu ya pamoja ni kutoka kwenye hatua ya kuweka misingi hadi kufanikisha matokeo dhahiri na kutekeleza kikamilifu sera ya kilimo ya kikanda ya SADC " alisema Bw. Diallo.

Naye Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) nchini Tanzania, Dkt. Nyabenyi Tito Tipo alisema kipindi cha miaka mitano iliyopita, maendeleo makubwa yametokea katika utekelezaji wa mifumo ya Usafi na Usalama wa Chakula (SPS) nchini Tanzania, licha ya changamoto ambazo zinaweza kuwa kikwazo katika kuingia kwenye masoko ya kimataifa kama Umoja wa Ulaya (EU), Asia, na masoko mengine.

"Katika kipindi hiki zaidi ya wakulima 200 wa parachichi wamefanikiwa kuuza mazao

yao nje ya nchi hasa kwenda Afrika Kusini na India. Washirika wa mafunzo pia wamelihakikishia kutokuwepo kwa virusi vya mafua hatari ya ndege (highly pathogenic avian influenza) nchini, pamoja na kutokuwepo kwa ugonjwa wa Fusarium wilt (ugonjwa wa ndizi), jambo ambalo limeimarisha usalama wa mimea." Alisema Dkt. Tipo

Aidha, kampeni ya chanjo ya Peste des Petits Ruminants (PPR) ilitekelezwa kwa mafanikio, ikiongeza nguvu katika mifumo ya afya ya wanyama. Msingi pia umewekwa ili kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya kuuza nje, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuuza bidhaa kwenda Mauritius." Aliongeza Dkt. Tipo.




# UJUMBE WA TANZANIA WASHIRIKI JUKWAA LA MIFUMO YA CHAKULA AFRIKA NCHINI SENEGAL

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena, ameongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika uliofanyika jijini Dakar nchini Senegal kuanzia Septemba Mosi hadi 5, 2025.

Jukwaa hilo limekutanisha Viongozi kutoka nchi mbalimbali wakiwemo, Marais, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Maafisa waandamizi kutoka sekta za mifumo ya chakula. Washiriki wengine ni pamoja na sekta binafsi, wadau wa maendeleo, vijana, wajasiriamali, wakulima, wafugaji na wavuvi.

Jukwaa hilo limebeba kauli mbiu isemayo Vijana wa Afrika Vinara wa Ushirikiano, Ubunifu na Utekelezaji wa Mageuzi ya Mifumo ya Chakula.

Bi. Agnes Meena ameongoza ujumbe wa Tanzania katika Majadiliano ya mada mbalimbali zikiwemo, ushirikiano wa kikanda na kitaasisi katika utekelezaji wa mpango Jumuishi wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP), vikao maalum vya Mawaziri wa sekta za mifugo Afrika na vikao maalum vya kujadili fursa za uwekezaji kwa nchi ya Tanzania.

Sambamba na hilo Katibu Mkuu amekutana na kufanya vikao na baadhi ya wadau wa Maendeleo (Bilateral Meetings) kwa ajili ya kujadili fursa za ushirikiano kando ya mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika.





# Tanzania yaikaribisha Oman kuwekeza Sekta za Mifugo na Uvuvi

**Na Daudi Nyingo**

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefungua milango ya uwekezaji kwa wafanyabiashara kutoka Oman, hatua inayolenga kuimarisha diplomasia ya kiuchumi iliyojengwa baina ya nchi hizo mbili kwa muda mrefu.

Ujumbe wa wafanyabiashara hao kutoka Oman ulioongozwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara na Viwanda katika Mkoa wa Al Wusta na Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Chama cha Biashara na Viwanda cha Oman, Dkt. Salem Al-Junaibi (Mb) uliokutana Septemba 9, 2025 na uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ukiongozwa na Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Prof. Mohamed Sheikh katika ukumbi wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Temeke jijini Dar es Salaam.

Mazungumzo hayo yalijikita katika kuangalia fursa za kuwekeza kwenye maeneo ya uchakataji wa nyama na samaki, ujenzi wa viwanda vya ngozi na maziwa, ufugaji wa kisasa wa samaki, uzalishaji wa chakula cha mifugo, uzalishaji wa chanjo za mifugo, pamoja na miradi ya baridi (cold chain facilities) kwa ajili ya kuhifadhi na kusafirisha mazao ya mifugo na uvuvi kwenda masoko ya kimataifa.


Katika ziara hiyo, ujumbe wa Oman uliambatana pia na Mkurugenzi wa Idara ya Mashariki ya Kati kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Abdalah Kilima.






# MATUKIO KWENYE PICHA

Wataalam na Viongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi walivyotekeleza majukumu yao katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchini katika mwezi Septemba, 2025.














MATANGAZO



## — BEI YA MBEGU ZA MALISHO
### (JUNCAO NA MAJANI TEMBO)

**Punguzo** Hadi 90%

**SHILINGI ~~4,000~~ → Sh. 1000**

**Kwa mawasiliano zaidi:**

Vikuge (Pwani) - 0714060849
Langwira (Mbeya) - 0757637241
TALIRI - 0655420703
LITA - 0742762364

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Wizara ya Mifugo Na Uvuvi




**Kwa mawasiliano zaidi:**

Kingolwira (Morogoro) - 0787493792
Mwamapuli (Tabora) - 0779154377
Ruhila (Songea) - 0659669227

www.mifugouvuvi.go.tz

# Jarida la Mtandaoni

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2870
Mji wa Serikali Mtumba
Dodoma , Tanzania
simu : +255 26 2322610
Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz

@wizara ya Mifugo na Uvuvi